

**MUHTASARI WA MAMBO YA KUFANYWA NA WENYE MADARAKA NGAZI YA HALMASHAURI ZA WILAYA, MIJI, MANISPAA NA MAJIFI**

Kuhuisha Sera Ngazi ya Halmashauri za Wilaya na Miji	<p><b>Sera ya Ardhi:</b> Kufuatilia utekelezaji wa wajibu wa kisera wa kutenga ardhi na maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za vijana.</p> <p><b>Sera ya Vijana:</b> Kufuatilia matakwa ya vijana kushiriki kwenye Majukwaa ya Vijana katika ngazi ya Wilaya na zile za chini.</p>
Kuhuisha Sheria na Kanuni Ngazi ya Halmashauri za Wilaya na Miji	<p><b>Sheria ya Ardhi:</b> Kufuatilia utekelezaji wa sheria ndogo na taratibu za kuwatengea vijana maeneo ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1977.</p> <p><b>Mfuko wa Maendeleo ya Vijana:</b> kutunga sheria ndogo kuadhibu wanaoshindwa kuwapelekea vijana na walemevu asilimia 5 ya mapato ya ndani ya HSM.</p> <p><b>Maeneo Maalum ya Soko:</b> Kusimamia sheria za masoko; na hasa zinazohitaji kuwa na maeneo maalum ya kuza bidhaa za kilimo (designated market places) na kutumia vipimo maalum vya ujazo na uzito; ikiw ni pamoja na kupiga marufuku matumizi ya "lumbesa".</p>
Kuboresha Mahusiano ya Kitaasisi katika ngazi ya Halshauri za Wilaya na Miji	<p><b>Vikundi vya Vijana view na Utamaduni wa Kuweka Akiba:</b> kuhamasisha juhudzi za kuunda vikundi vya vijana na kuwafundisha umuhimu wa kuweka akiba ili iwe rahisi kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mikopo.</p> <p><b>Kuwakaribisha wadau wa sekta binafsi wenye nia</b> ya kuunga mkono miradi na biashara za vijana.</p> <p><b>Kuboresha uratibu wa kuwapa elimu vijana juu ya faida ya mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani</b> kwa ajili ya mauzo ili kusubiria bei nzuri zaidi ya soko kuliko kuza mara tu baada ya kuvuna.</p> <p><b>Kuratibu mfumo wa kuanzisha majukwaa ya vijana</b> ngazi ya wilaya, kata na vijiji.</p> <p><b>Vijana kupewa fursa ya kuchangia maoni yao</b> wakati wa kuandaa mipango ya maendeleo</p>
Mabadiliko ya Fikra na Mitazamo juu ya Kilimo na Kilimo-Biashara	<p><b>Kuanzisha makala ya vipindi na kutumia magazeti, redio za kijamii na runinga (TV)</b> kwa ajili ya kubadilishana maoni ya wazazi juu umuhimu wa kuwasaidia vijana; na pia kubadilisha mtizamo hasi wa vijana kuwa kilimo hakina faida.</p> <p><b>Kuwafundisha na kuwashimiza vijana kutumia TEHAMA (ICT)</b> katika kutafuta taarifa mbalimbali za masoko, teknolojia na mifumo ya kibashara.</p> <p><b>Kuwatambulisha na kuwaunganisha vijana na Watu wa Mfano wa Kuigwa</b> (role models) waifanikiwa katika kilimo-biashara ili kuchochaea hamasa ya vijana. Watu kama hao ambaa ni kama kioo cha jamii wanawenza kukanibishwa kwenye vikao vya Majukwaa ya Vijana.</p>

Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji zinapaswa kushinikiza Taasisi za Kitaifa (kama Wizara na Bunge) kufanya mageuzi juu ya (a) sera na sheria za kuhitaji Mabenki kutenga sehemu ya mapato yao kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (MMV); (b) kuajiri wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kuwafundisha vijana stadi na elimu mbalimbali na hasa elimu ya biashara na fedha; (c) mitaala ya elimu ya kilimo kufundishwa shule za msingi na sekondari; (d) makampuni binafsi kuwekeza sehemu ya mapato yao katika miradi ya vijana kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii; na (e) kufungua matawi ya VETA na SIDO kwenye wilaya zote ili kurahisisha upatikanaji wa kozi na kupunguza gharama zake.



## East Africa Youth Inclusion Program

In partnership with



### The Economic and Social Research Foundation (ESRF)

51 Uporoto Street, Ursino Estate. P.O Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania  
 Mobile: +255-754 780133, +255-655 780233  
 Tel: +255-22 2926084 - 90  
 Fax: +255-22 2926083  
 E-mail: esrf@esrf.or.tz or info@esrf.or.tz  
 Website: http://www.esrf.or.tz



No. 12/2017 - Swahili Version

# ESRF POLICY BRIEF



ECONOMIC AND SOCIAL RESEARCH FOUNDATION

www.esrf.or.tz

## Mradi wa Kuboresha Mazingira Wezeshi ya Kuongeza Ushiriki wa Vijana Kwenye Shughuli na Biashara katika Sekta ya Kilimo Tanzania

### TAMKO LA SERA ZA KWASADIA VIJANA KWENYE KILIMO BIASHARA

#### WAJIBU NA MCHANGO WA HALMASHAURI ZA WILAYA

Imeandikwa na: H.Bohela Lunogelo, Fortunata Makene, Patrick Tuni Kihenzile and Richard Ngilangwa

Idadi ya Vijana ni zaidi ya nusu ya idadi ya wananchi wa Tanzania. Wengi wanatambua fursa zilizopo kwenye kilimo-biashara kwa vile mahitaji ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla yanazidi kuongezeka sambamba na uongezeko la idadi ya watu ambao wako kwenye sekta zingine nje ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. ESRF imefanya utafiti ambao unadhihirisha wazi kuwa ili vijana waweze kushiriki kikamilifu na kutoa mchango mzuri kwenye uchumi wa Halmashauri zetu, itabidi kuzingatia maswala ya kisera na kiutendaji yafuatayo:

#### A-Wenye madaraka (duty bearers) katika Halmashauri na Serikali za Mitaa (HSM) itabidi wawe mstari wa mbele kuhimiza mambo yafuatayo:

- ✓ Kutenga ardhi na maeneo maalumu kwa ajili ya kilimo biashara na viwanda vidogo na vya kati kwa ajili ya vijana wanaopenda kilimo-biashara, usindikaji na biashara zingine.
- ✓ Baraza la Madiwani kusimamia na kufuatitia utekelezaji wa matakwa ya kisheria kuwatengea vijana asilimia 4 ya mapato ya ndani ya HSM. Ni pamoja na asilimia moja kwa ajili ya Vijana wenye ulemavu.
- ✓ Kuvutia wadau wa sekta binafsi (WSB) kujenga vyuo vya ufundi, karakana na viwanda vidogo vidogo na vya kati (VVVK) kwa kusajiliwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundji (VETA) na shirika la viwanda vidogo (SIDO) ili kuwapatia vijana ujuzi na weledi unaotakiwa kwenye kilimo-biashara na usindikaji bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi
- ✓ HSM kupitisha sheria ndogo inayoitaka Idara ya

Maendeleo ya Vijana kuanzisha Dawati Maalumu la Kuwasaidia Vijana wanaopenda kuijunga na kilimo au kwenye sehemu ya mlolongo wa uongezaji thamani mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Kuwaunganisha Vijana na Makundi yao na Kampuni za Tehama ili vijana waweze kujifunza na kutanua uelewa wao kwenye fani mbali mbali za kitaaluma (e-learning), elimu masoko (e-marketing) na elimu biashara (e-commerce) kwa ajili ya kuboresha ufanisi katika uzalishaji na biashara zao.

Kuhamisha matumizi ya mfumo shirkishi ili kupata michango ya mawazo ya vijana katika kutetea maslahi yao. Hii itahusisha, pamoja na mambo mengine uundwaji wa Majukwaa ya Vijana katika ngazi za Vijiji, Wilaya na Mikoa.

Ili kubadili fikra za vijana kuwa na mtizamo chanya juu ya kilimo-biashara HSM zinasaidia uanzishwaji wa vikundi vya kijamii vinavyojishughulisha na ngoma, maigizo na vyombo vya habari kama magazeti, redio, runinga na mitando ya kijamii.

**Utangulizi**

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 imetilia mkazo umuhimu wa kuweka mazingiza mazuri ya kuwawezesha vijana kujihusisha na shughuli za kiuchumi, ikiwemo kilimo cha kisasa na kibiashara. Kwa maana hiyo, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manisapaa na Majiji (HSWM) zinatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia vijana wake kupata maeneo ya kulima mazao, kufuga mifugo, kufanya biashara za mazao, na kujenga viwanda vidogovidogo. Uwezesha jiji wa vijana kujihusisha na shughuli za kilimo na biashara kutasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira. Kwa sababu vijana wengi wataweza kujiajiri na kuachana na mipango ya kukimbia mijini. Kwa bahati nzuri kuna miradi ya serikali na wafadhili kama HEIFER International kuitia mradi wa "Kuwajumuisha Vijana wa Afrika Mashariki katika kilimo biashara" (*East Africa Youth Inclusion Program (EAYIP)*). Mradi huu unatambua umuhimu wa kuchoea ushiriki wa vijana kwenye shughuli za uchumi vikiwemo kilimo cha kibiashara na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Mradi utaanza na kata/vijiji vichache teule katika halmashauri za Iringa Vijiini, Kilolo, Mufindi, Mafinga Mji, Njombe Mji, Njombe Wilaya, Wanging'ombe, Mbeya Wilaya, Rungwe Wilaya, Busekelo Wilaya, na Mbozi Wilaya.

**Hali Halisi ya Changamoto za Ajira kwa Vijana**


Takwimu za Kitaifa za mwaka 2012 zinaonesha kuwa theluthi moja ya Watanzania wote ni vijana wa umri wa miaka 15 hadi 35. Zaidi ya robo tatu (asilimia 76.2 hadi 79.4) ya vijana kati ya miaka 15 hadi 34 wanategemea shughuli za kilimo kujipatia kipato (angalia grafu na.1). Mradi wa Heifa wa Kujuimusha Vijana kwenye Uchumi (EAYIP) unalenga kundi kati ya miaka 15 na 24, ambao pia hutegemea kilimo kujikimu.

**Sera za Taifa Kuwawezesha Vijana Kiuchumi**

Sera ya Maendeleo ya Vijana inatoa mwongozo wa kuwawezesha vijana kwa kuwabadiishi fikra na kuwapatia ujuzi na stadi za kazi, raslimali na mitaji ili waweze kujishughulisha na kufanikiwa kiuchumi, ikiwemo sekta ya kilimo. Sera zingine za kitaifa zinazohimiza vijana kujihusisha na kilimo biashara ni pamoja na rasimu ya 2017 ya Sera ya Taifa ya Ajira (ipo kwenye matayarisho) na Mkakati wa Kitaifa wa Kuwahusisha Vijana Kwenye Kilimo 2016-2021. Sera hizi zinahimiza serikali kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii ili vijana waweze kutumia vizuri elimu, ujuzi na stadi zao kujiajiri na pia kuajiri vijana wenzao. Kwa mantiki hiyo, halmashauri zetu zina wajibu wa kutafsiri sera hizo na kutafuta mbinu za kuwawezesha vijana wake kiuchumi kwa kuangalia maliasili zilizoko kwenye wilaya, mji, manispaa au jiji husika.

**Je Halmashauri au Serikali za Mitaa Zina Wajibu Gani?**

Mabaraza ya Madiwani na Wakuu wa Idara mbalimbali watashirkiana kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatenga bila kukosa asilimia 5 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (MMV); ambapo katika hizo asilimia 20 zinakuwa kwa ajili ya vijana wenyewe ulemavu wa viungo. Kuna ushahidi kuwa halmashauri zingine hazipeleki michango yote ya asilimia 5 ya mapato ya ndani kwenye MMV. Jambo hili ni kwa mijibu wa sheria ya nchi kwa hiyo inapaswa kutekelezwa bila kutoa kisingizio kuwa "kilichokusanywa hakitoshi kwa shughuli zingine za halmashauri". Pesa zitolewazo kwa Vikundi vya Vijana, ambapo wanachama wao huanzia watu watano, huwa kidogo sana kiasi kwamba hazitoshi kuleta matokeo chanya ya kuizalishaji au kibiashara. Kuna umuhimu wa kubadilisha mkakati ili vikundi vipewe mtaji wa kutosha kuviwezesha

**Grafu 1-Chanzo Kikuu Cha Kipato Kwa Vijana**

kufanya mabadiliko ya kweli kiuchumi na kibiashara. Kuna maoni kuwa ni heri kulenga vikundi vichache vitakavyofanikiwa; kuliko kujipatia pesa vikundi vingi pesa kidogo ambazo haziwezeshi kufanya mabadiliko ya kiuchumi. Vijana waliohojiwa na mradi huu wa EAYIP walionyesha kujihusisha na ufugaji wa kuku wa mayai na nyama, mbuzi, nguruwe na biashara za kuuza mazao (pamoja na maziwa) na bidhaa zingine za viwandani kwa ajili ya wanavijiji.

**Je Vijana Wanakabiliana na Changamoto Gani?**

Mwaka 2017 wakati wa matayarisho ya huu Mradi wa Kuwajumuisha Vijana wataalamu wa ESRF waliambiwa na vijana changamoto na matarajio yao katika kujihusisha kwenye kilimo biashara kama ifuatavyo:

(a) Kukosa mitaji ya kupanua kilimo-biashara na kutumia mbinu za kisasa zaidi; (b) Baadhi ya vijana kutojua kuwa kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (MMV) wa Wilaya na masharti yake. Waliohahi kukopa walisema pesa zinazotolewa ziliikuwa kidogo mno kukidhi mahitaji; (c) Elimu na uelewa mdogo wa mbinu na teknolojia ya kilimo cha kisasa na kibiashara, kutambua masoko na kutayarisha miradi inayokubalika na taasisi za kifedha; (d) Kukosa ardhi ya kufanya shughuli za kilimo-biashara kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na mila na desturi; (e) Masharti magumu ya kupata mikopo (kama vile riba kubwa na kuweka dhamana ya mali isiyohamishika); (f) gharama kubwa ya pembejeo na zana za kilimo; (g) vijana kubaguliwa kwenye mgao wa ruzuku ya pembejeo za kilimo; (h) bei ndogo ya kuuzia mazao ambayo haileti faida kwa mzalishaji; (i) kubadilika bei ndani ya msimu ikiwa ndogo mno mara tu baada ya kuvuna; na (j) kuwazuwa wakulima na wafanya biashara kuuza mazao nje ya nchi kwa faida zaidi kuliko soko la ndani ya nchi.

Halmashauri zinatakiwa kuziunga mkono Serikali za Mitaa na Vijiini katika kutua changamoto zingine kama vile: (a) wazazi kukataa kuwasaidia vijana kuanzisha

biashara; (b) fikra za vijana wengi kudhani kilimo hakina faida; (c) kukosa jukwaa au utaratibu wa vijana kutoa na kubadilishana mawazo ya kimaendelo na viongozi wa kijiji na kata. Hii ni pamoja na kuwapa fursa vijana kutoa maoni yao kwenye mikutano inayoitishwa na viongozi wa kiserikali na kisisasa.

**Matumaini Makubwa ya Vijana Mbele Yetu**

Vijana wanapaswa kuchukua fursa ya ongezeko la kasi la watu ambao wanategemea ajira maofisini na viwandani na hawalimi. Hawa wote wanahitaji chakula, matunda, vinywaji, nguo, viatu, nyumba na mawasiliano. Kundi la wafanyakazi wa kipato cha kati na cha juu linazidi kuongezeka, hivyo ni soko zuri kwa bidhaa ambazo vijana wanazalisha au kuuza. Mradi wa umeme vijiji unatoa fursa kuanzishwa viwanda vidogodogo vijiji. Taasisi za kifedha kama CRDB, NMB na NBC pia zimeanza kuwasaidia wajasiriamali.

**Je Halmashauri Zitawasaidia Vipi Vijana Wake?**

Halmashauri zetu zinalo jukumu la kuhamasisha Serikali za Mitaa na Vijiini kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya miradi ya vijana kwenye kilimo, viwanda na biashara. Hili ni sharti nyeti sana na muhimu kama kweli Halmashauri zetu zina dhamira ya kweli ya kuwasaidia vijana wajijingize na kufanikiwa katika kilimo-biashara.

Viongozi wa Idara Mbalimbali katika Halmashauri wawasaidie vijana kuanzisha makundi ya kiuchumi na kuunda Jukwaa la Vijana ili kubadilishana mawazo. Halmashauri zipange kwa makusudi kabisa kuleta wataalamu na taasisi za kuvisadia Vijiini kuandaa mafunzo ya kuwajengea uwezo vijana kuwa na ujuzi na stadi za kushiriki kwenye kilimo biashara. Vijana wanahitaji kusaidiwa kubadili fikra na kuwa na mtizamo chanya kuhusu kilimo biashara. Jambo hili linawenza kufanywa kwa kutumia Vikundi vya Sanaa za Maonyesho na Ziara za Mafunzo sehemu nyingine nchini na nje ya nchi.